❖ MKONGE NI NINI?

Mkonge au kwa jina lingine Katani ni moja ya mazao mkakati yaliyoonesha mafanikio makubwa katika nchi ya Tanzania na hii ni kutokana na uwezo wake wa kuhimili hali ya ukame ambayo huwa ni changamoto kubwa kutokana na mabadiliko ya tabia nchi yanayopelekea ukame, zao hili linalimwa kwa kiasi kikubwa maeneo ya Tanga na Morogoro.

Mkonge ni zao la kibiashara ambalo huzalisha nyuzi(sisal fiber)ambapo nyuzi hizi hutumika katika kutengeneza bidhaa mbalimbali kama vile kamba, mazulia(*kapeti*), magunia, mavazi, nywele, geotextiles, gypsum boards, decoration,pombe(*tikila)* nk

Mkonge pia hutumika katika kuzalishia umeme ambao unaweza tumika na jamii kiujumla. Mfano mzuri wa uzalishaji huu wa umeme unapatikana kwenye mradi uliopo Ngomeni Tanga.

Zao la Mkonge huanza kuvunwa baada ya miaka 2.5 mpaka 3 shambani lakini kama utatunzwa vizuri tofauti na hapo unaweza kukaa mpaka miaka 4 ndio uwe tayari kwa kuvunwa. Lakini pia kiujumla Mkonge unaweza kuishi shambani mpaka miaka 15.

Ikumbukwe kuwa Mkonge ni zao ambalo ni gumu kuathiliwa na kushambuliwa na wadudu shambani tofauti na mazao mengine.

TIBF



TIBE



TIBF

❖ MBEGU ZA MKONGE

Kiujumla mbegu za Mkonge hupatikana katika njia mbili nazo ni;-

i. Njia ya Machipukizi/maotea *(suckers*)

ii. Njia ya vikonyo kwenye vitalu (*bulbis*)


i. Njia ya Machipukizi/maotea *(suckers*)

Hizi ni aina ya mbegu ambazo huchipukia kutoka kwenye shina na pembezoni mwa Mkonge uliyo komaa. Mfano wa aina hii ya mbegu ni

kama vishina vya mgomba vinavyo chipukia.

Hapa mkulima anaweza kwenda kuchimba mbegu hizi kwenye mashamba ya Mkonge uliokomaa na kwenda kupanda shambani kwake ila ni lazima uzingatie ukubwa wa mbegu husika na jinsi ya kuichimba. Haishauriwi kuchimba mbegu iliyo komaa sana wala mbegu changa sana. Pia lazima mbegu uichimbe ikiwa na mizizi yake ili iwe rahisi kushika na kukua shambani.

Katika maeneo yenye mashamba makubwa wanakijiji walio karibu huingia mashambani na kuchimba mbegu hizi kwa lengo la kuuza kwa wahitaji na kwa waastani mbegu za aina hii huuzwa kati ya Tsh 30 mpaka Tsh 50 kwa kila mbegu/mche .




Mbegu za machipukizi
kutoka shambani

ii. Njia ya Vikonyo (*bulbis*)

Aina hii ya mbegu huota katika mlingoti wa Mkonge ulio komaa shambani baada ya maua ya Mkonge kupukutika. Mbegu hii huchukuliwa na wataalamu na kwenda kuandaliwa kwenye vitalu (*nursuring*) kwa uangalizi zaidi wa kitaalam na baada ya muda husika mbegu hizi huhamishiwa kwenye mashamba husika. Mfano wa mbegu hizi ni kama mbegu za vitunguu jinsi zinavyoandaliwa na mwisho kupelekwa shambani, mbegu za aina hii hupatikana sehemu kama **Mlingano Muheza Tanga.**

Aina hii ya mbegu ya mkonge hupatikana kwa Tsh100 mpaka Tsh200 kwa kila mbegu. Vile vile aina hii ya mbegu huuzwa kwa bei ya juu kidogo kwasababu huandaliwa na kupatikana tofauti. Mbegu ya vikonyo ndio mbegu bora kwani huandaliwa kitaalamu na pia humpa mkulima mazao mengi ndani ya muda mfupi, lakini pia ina uwezo wa kuishi kwa muda mrefu ukilinganisha na mbegu ya machipukizi.



❖ UPANDAJI NA UTUNZAJI WA MKONGE

i. Upandaji wa mkonge shambani

Baada ya kumaliza maandalizi ya kusafisha shamba basi ni vizuri kujua mfumo sahihi utakaotumika katika upandaji wa zao la Mkonge. Upandaji wa zao la Mkonge hufanyika kwa aina mbili tofauti ambazo ni ***Single Line Planting*** na ***Double line Planting***

i. Single Line Planting

Aina hii ya upandaji wa mkonge hupandwa mstari mmoja na kuacha nafasi katikati ya kila mstari wa mkonge shambani (*miraba*). Njia hii ya upandaji Wataalam hutumia vipimo mbalimbali ambavyo hutumika na kurahisisha upandaji wa zao hili. Mfano umbali wa shina moja na shina lingine,ukubwa wa nafasi kati ya kila mstari wa mkonge. Kiujumla njia hii huwezesha upandaji wa miche 3000 - 3500 kwa heka moja shambani.



ii. Double line Planting

Hapa mkonge unapandwa kwa mistari miwili na kuacha nafasi katikati ya kila hiyo mistari miwili iliyo karibu. Aina hii ya upandaji hutegemea sana vipimo na endapo makosa yatafanyika katika upandaji wake basi ni ngumu sana kuja kurekebisha makosa pale Mkonge unapokua mkubwa. Hivyo basi inashauriwa kupata

Mtaalam/Wataalam aliye na uwezo wa kufanya zoezi la upandaji kwa kutumia vipimo vilivyo sahihi katika shamba. Kiujumla njia hii huwezesha upandaji wa miche 4000 - 5000 kwa heka moja shambani.

Aina zote hizi hutumika kwa sababu tofauti lakini mara nyingi watu hupendelea sana upandaji wa double line kwa sababu unaweza kupanda miche mingi ndani ya heka moja kulinganisha na upandaji wa single line. Katika upandaji wa double line mavuno yake huwa ni ya wingi tofauti na upandaji wa single line. Uzuri wa upandaji wa single line ni rahisi kwenye upaliliajii wa shamba, lakini pia huwezesha Mkonge kukua kwa uharaka na mashina yake huwa ni makubwa na hii hupelekea uvunaji wa Mkonge uliokomaa vizuri kwa mda mfupi kwasababu mkonge unapata nafasi ya kukua vizuri kutokana na umbali wa mche na mche.

TIBE



❖ Utunzaji wa Mkonge shambani

Ili mkulima aweze kupata mavuno ya kutosha ya zao la Mkonge inashauriwa awe ameandaa shamba lake vizuri kabla ya upandaji, lazima shamba liwe na rutuba ya kutosha na pia mazingira mazuri yenye mvua, japo kuwa mkonge hauhitaji mvua nyingi kama mazao

mengine lakini ni muhimu kupata mvua hata kwa uchache pale mkonge unapokua mchanga. Kwamkonge ulio komaa unaweza kukaa hata zaidi ya miezi sita bila mvua na ukaendelea kuishi.

Utunzaji wa zao la Mkonge mara nyingi inategemea njia salama na sahihi za upaliliaji kwa kuondoa majani au magugu ili kuepusha kutumia maji na virutubisho vinavyotakiwa kutumika na mmea wa Mkonge. Na hii kwa kawaida mkulima anashauriwa apalilie shamba lake kila baada ya miezi sita (6) kwa mwaka yaani mara mbili kwa mwaka. Kwa Mkonge uliomchanga basi ni vyema mkulima apalilie shamba lake kila baada ya miezi minne (4) ili kufanya mmea ukuwe vizuri na kukomaa kwa uharaka shambani .

Inashauriwa kwa mkulima kupanda mazao ya mda mfupi kama mahindi, pamba, alizeti nk katika miraba ya mkonge iliyopo shambani, ili pale anapofanya upaliliaji wa haya mazao basi Mkonge pia huwa katika mazingira mazuri ya ukuaji na hii pia itamfanya mkulima kuwa na matunzo mazuri ya shamba lake na zao la mkonge kwa ujumla na kumuongezea kipato pale atakapovuna mazao mengine ya mda mfupi.





TBF



TIBF

❖ UVUNAJI WA MKONGE

Baada ya mkonge kukaa shambani kwa muda husika, Mkulima anatakiwa kujiridhisha kama Mkonge umekomaa vizuri kwa kuzingatia vitu kama jani la Mkonge liwe na urefu wa zaidi ya cm 60 na ni lazima majani yakatwe kwenye shingo yake na sio juu ya shingo, lakini pia mkulima atatakiwa kuvuna majani yaliyozidi nyuzi 45 na si vinginevyo.

Uvunaji wa Mkonge huvunwa kwa kipimo cha (***Mita***), ili mita ya majani ya Mkonge ikamilike ni lazima kuwe na mizigo ya majani ya Mkonge 110 na kwa kila mzigo mmoja huwa na jumla ya majani 30 ya Mkonge. Kwahiyo ili mita ikamilike ni lazima kuwe na mizigo 110 na kila mzigo uwe na majani 30.Kwa hapa mahesabu ya uvunaji wa Mkonge kiujumla huwa ni kwa mita na hata malipo ya wakataji wa majani ya mkonge shambani hulipwa kwa mita.

Kwa kitaalamu mkonge unatakiwa kuvunwa /kukatwa kila baada ya miezi minne ,yaani mara 3 kwa mwaka mmoja, hili litafanikiwa endapo utaratibu wa uvunaji utafatwa (yaani kuvuna majani yaliyozidi nyuzi 45 tu), kinyume na hapo mavuno ya mkonge yakizidishwa kwa mvuno mmoja huathiri mda wa ukuaji wa mkonge shambani, hivyo basi hupelekea mkulima kusubiri mda mrefu na husababisha mkulima kuvuna mara mbili kwa mwaka mkonge wake ,lakini kwa wakulima wengine huamua kuvuna mkonge wao mara moja tu kwa mwaka ili wapate mavuno mengi kwa wakati mmoja ,kiujumla wastani wa mavuno ya mkonge huwa ndani ya kila baada ya miezi minne au kila baada ya miezi sita kwa wakulima wengine ,mvua na ardhi yenye rutuba pia huathiri sana ukuaji na mda wa uvunaji wa mkonge kwa kiasi kikubwa shambani.

TIBF


Mkataji akikata/
kuvuna mkonge



TIBF

❖ MASHINE ZINAZOTUMIKA KUCHAKATA MKONGE

Hizi ni mashine ambazo hutumika kuchakata majani ya Mkonge na kuwa nyuzi (***Sisal Fiber)*** au nyuzi za katani. Muonekano wa machine hizi hutofautiana kulingana na ubunifu na utashi wa mtengenezaji lakini hizo zote huangukia katika aina hizi tatu za mashine za uchakataji wa Mkonge ambazo ni ***Raspado sisal machine***, ***Mobile sisal machine*** na ***Corona sisal machine***

i. Raspado sisal machine

Hii ni mashine ndogo ya mkono inayotumia mafuta ya *Diesel* kuchakata Mkonge. Mashine hii huendeshwa na watu wa nne (4) mpaka watano (5) kwenye uchakataji wake. Aina hii ya mashine

huzalisha grade ya nyuzi aina ya **SSUG** tu, jani moja moja huingizwa kwa mkono kwenye mashine na kutolewa ili kupata nyuzi, kwa zoezi hili mashine hii inaweza kusagisha/kuchakata mita tano (5) mpaka nane (8) kwa siku. Idadi ya mita za mkonge huchakatwa kulingana na speed na uzoefu wa wafanyakazi wanaoendesha mashine hiyo.

Baada ya nyuzi kupatikana huoshwa na maji masafi pembeni na kwenda kuanikwa juani.



TBF

ii. Mobile sisal machine

Hii ni mashine kubwa ya kuchakatia Mkonge inayotumia machine kubwa ya mafuta ya *Diesel* au monta ya umeme kuendeshea mtambo

wa kuchakatia Mkonge. Mashine hii huzalisha grade ya juu **UG** na kwa uchache grade ya **SSUG**.Mashine hii huwa na uwezo wa kuchakata mita mpaka 50 kwa siku, na baada ya nyuzi kuchakwatwa huoshwa na kuanikwa juani. Mashine hii inaweza kuhamishika kutoka sehemu moja kwenda nyingine ***(moverable machine) .***



Machine ya mobile

iii. **Coronal sisal machine**

Hii ni mashine kubwa inayotumia umeme yenye uwezo wa kuchakata Mkonge mwingi kwa siku mpaka mita 150. Pia mashine hii huwa na mifumo ya maji ya kuoshea Mkonge moja kwa moja yaani unaingiza majani ya Mkonge upande mmoja na kupokea nyuzi safi iliyochakatwa na kuoshwa na maji ya presha upande mwingine tayari kwa kuanikwa. Mashine hizi hutumia umeme kujiendesha na mara nyingi hizi mashine hutumika na makampuni yenye mashamba makubwa ya Mkonge. Vile vile mashine hizi huzalisha nyuzi zenye ubora sana yaani grade za juu kama **UG** na ni mashine kubwa ambayo hufungwa sehemu moja tu na ni ngumu kuhamishika kirahisi .

TIRF



TIBE



TIBF

❖ GRADE ZA NYUZI YA MKONGE (*SISAL FIBER*)

Grade za nyuzi za Mkonge hupatikana baada ya zoezi lijulikanalo kama kupiga kayamba(*kubrush nyuzi kwenye machine*) kumalizika, ndipo nyuzi hizi huchambuliwa na kupangwa kulingana na ubora wake. Kwa kawaida uzalishaji wa nyuzi za Mkonge hufanyika kwa kuzingatia grade tatu (3) ambazo ni **UG, SSUG,** na **TOW** na ndizo zinazotumika sana na wadau wengi wa Mkonge.

Inafahamika na Watalamu kuwa kuna grade zaidi ya hizo na kwa mpangilio ni kama ifatavyo **Grade 1, Grade 2, 3L, 3S, UG, SSUG** na **TOW.** Lakini kwa asilimia kubwa hizo grade 3 ndio huzalishwa na kutumika kwa sana hapa Tanzania.

i. UG sisal fiber

Hizi ni nyuzi(*fiber*) zenye ubora na ambazo huzalishwa kwa mashine kubwa tu. Nyuzi hizi zinatakiwa kuwa na urefu usiopungua 60cm na zinatakiwa kuwa na rangi nyeupe au rangi ya (brown) kidogo zisizo kuwa na madoa ya aina yeyote.Vilevile hazitakiwi kuwa na ukijani au rangi ya aina yeyote ile, kiujumla hizi ni nyuzi ambazo soko lake liko juu na zina bei nzuri sana sokoni.





ii. SSUG Sisal fiber

Hizi ni nyuzi (*fiber*) ambazo zinatakiwa kuwa na rangi ya weupe kidogo lakini pia nyuzi hizi huwa na ukijani kwa uchache na madoa ya rangi nyeusi (*black spot*) kwa baadhi ya nyuzi. Aina hii ya nyuzi ni grade iliyo chini ya UG na ubora wake ni wa wastani na soko la SSUG ni kubwa na bei yake huwa nzuri pia.

TIBF



iii. TOW

Hii ni grade ya mwisho kabisa kwenye nyuzi za Mkonge na aina hii hupatikana baada ya kubrash nyuzi kwenye mashine (kayamba) ya kuchania nyuzi. Aina hii ya nyuzi pia hujulikana kama mabaki yatokanayo na zoezi la kayamba. Mabaki ya nyuzi ya UG hutoa grade 1 ya TOW na hii ni kutokana na ubora na usafi wa grade ya UG. Mabaki ya SSUG hutoa grade 2 ya grade ya TOW na grade hii pia ina soko na bei yake ni ya kawaida.

TIBF



❖ BIASHARA YA MKONGE (*SISAL FIBER*) KWA PANDE ZOTE.

Kipengele hichi kinaelezea manufaa ya kiuchumi (*pesa*) ambayo mtu anaweza kuyapata kupitia kilimo cha Mkonge kuanzia shambani mpaka nyuzi (*fiber*)zinapo safirishwa kwenda masoko ya duniani ni

kama ifuatavyo;-

I. Mkulima wa Mkonge

Kwenye kilimo cha Mkonge mkulima anaweza kupata kipato katika njia kuu tatu. Njia ya kwanza ni pale mkulima anapoamua kupanda mazao mengineyo wakati wa utunzaji wa shamba la Mkonge na hapa hujiongezea kipato pale anapovuna mazao hayo. Njia ya pili ambayo ndio kiini cha kilimo hiki kwa mkulima ni uuzaji wa majani ya Mkonge kwenye viwanda vya uchakataji. Mkulima huuza Mkonge wake kwa kipimo cha mita kwa wenye viwanda vya uchakataji na kwa wastani wa heka moja ya shamba la Mkonge mkulima anaweza kupata mita 17-25 ,na kwa wastani wa bei ya mvuno/mkato wa kwanza huwa ni sh 5,000- 8,000 kwa kila mita, kwa mkato wa pili bei huwa ni kati ya sh 10,000-13,000 kwa kila mita moja na kwa mkato wa tatu bei huwa sh 15,000-18,000 kwa mita moja.

Mivuno/mikato inayoendelea huwa ni maelewano ya mkulima na Mmiliki wa kiwanda kulingana na jinsi Mkonge ulivyokua na kukomaa shambani mfano mkato wa 6,7 nakuendelea mita moja huuzwa mpaka sh 45,000 na ndio bei inayotumika kwa sehemu nyingi za Mkonge. Mkonge unaoanza kukatwa huwa ni mdogo kidogo na majini yake sio marefu sana lakini yaliyokomaa ndio maana bei huongezeka kadri mavuno yanavyofanyika kwasababu majani hukua na kukomaa zaidi. Vilevile zao la Mkonge hukua kulingana na muda unaokaa shambani, ila kiujumla bei huwa ni ya maelewano kati ya mkulima na mnunuzi kulingana taratibu na kanuni zote za kibiashara.

Mkulima mwenye heka 10 anayevuna mita 20 kwa heka, mvuno wake wa kwanza anaweza kupata mita zaidi ya 200 shambani kwake na kwa wastani wa Tsh 7,000 kwa mita, mkulima huweza kuingiza Tsh 1,400,000 (200*7,000), kwa mkato wa pili mita 200 kwa Tsh12,000 mkulima anaweza kupata Tsh2,400,000 (200*12,000), na kwa mkato wa tatu kwa bei ya 16,000 kwa mita mkulima anaweza kupata

Tsh3,200,000 (200*16,000). Kiujumla mkulima ndani ya mwaka wa mavuno anaweza pata Tsh7,000,000 na zaidi kwa mwaka wa kwanza wa mavuno, mkulima anapofikia hatua ya kuuza Mkonge wake kwa bei ya Tsh40,000-50,000 kwa mita anaweza pata zaidi ya Tsh10,000,000 (mita 200*50,000) ndani ya mvuno mmoja, na kwa mwaka ikitokea akavuna mara tatu anaweza kupata hadi Tsh 30,000,000.

Kwa mkulima mwenye heka 100 (hekta 40) anaweza kupata jumla ya mita 2,000 shambani kwake kwa mvuno mmoja. Mvuno wa kwanza anaweza kupata Tsh14,000,000 (2,000*7,000), mvuno wa pili mkulima anaweza kupata zaidi ya Tsh 24,000,000 (2,000*12,000) na mkato wa 3 pia anaweza kuingiza zaidi ya Tsh 32,000,000 (2,000*16,000). Kwahiyo ndani ya mwaka wa kwanza wa mavuno mkulima anaweza kupata Tsh70,000,000 na akiweza kufikia muda wa kuuza Mkonge wake kwa bei ya Tsh 40,000- 50,000 kwa kila mita anakuwa na uwezo wa kupata zaidi ya Tsh80,000,000 (2,000*40,000) na kwa mwaka kama atavuna mara tatu basi anaweza kupata zaidi ya Tsh 240,000,000.

Ifahamike kuwa zao la Mkonge pia hufikia kikomo cha ukuaji wake shambani lakini majani yake huendelea kuchanua kila unapokatwa/kuvunwa. Kutokana na ukomavu wake hupelekea Mkonge kutokuongezeka tena na hapo ndio mkonge huanza kutoa malingoti kwenye mashina yake hii ikiwa ni ishara ya kuanza kuzeeka kwake. Baada ya malingoti kutoka bado mkulima anaweza kuvuna Mkonge wake zaidi ya miaka 5 mpaka 7 mbele.

Njia ya tatu inayo muwezesha mkulima kupata kipato ni kwa kuuza malingoti baada ya kukua vizuri na kukomaa hapo akiwa anaendelea kuvuna Mkonge wake kama kawaida. Lingoti hutoka mara moja tu kwa kila shina katika maisha ya mkonge hivyo basi mkulima inaweza kumuongezea kipato.

Mkulima hatoingia gharama yeyote ya uvunaji wa mkonge wake kama ataamua kuuza majani yake, gharama zote za uvunaji zitakua

chini ya mnunuzi mwenyewe na hapa ni baada ya Mkonge kukatwa. Mkulima huhesabu mita zake shambani na kupokea malipo yake kutoka kwa mnunuzi kulingana na bei waliyo kubaliana na gharama pekee ambayo mkulima ataingia ni kusafisha shamba lake pale majani na magugu yanapoota, hii ni kwa kipindi chote cha uhai wa Mkonge .

Mkulima mwenye uwezo wa kununua mashine na kuchakata Mkonge wake mwenyewe ni vizuri sana maana itamuongezea faida nzuri zaidi kuliko kuuza majani na hii mara nyingi hufanywa na wakulima wenye mashamba makubwa mfano zaidi ya heka 40, hapa hutegemeana na ukubwa wa shamba na hali ya kiuchumi ya mkulima ya kuweza kuendesha shughuli za uchatakaji wa Mkonge yeye mwenyewe.

Mkulima kwenye zao la mkonge kiujumla ana maamuzi ya kuuza majani/mkonge wake kwenye viwanda na kupokea malipo kutokana na idadi ya mita zilizopatikana shambani kwake kwa bei ya maelewano ,mkulima pia ana nafasi ya kununua mashine ndogo kwa lengo la kuchakata mkonge wake yeye mwenyewe na kupata faida zaidi, na kwa wale wakulima wenye mashamba makubwa na wenye uchumi nzuri wanaweza kukodisha mashine kubwa ya mobile kwa lengo la kuchakata mkonge wao ili wazalishe grade ya juu zaidi (UG) na kujipatia kipato kizuri zaidi.

II. Mmiliki wa Kiwanda kidogo cha Mkonge

Huyu ni mfanyabiashara anayemiliki kiwanda kidogo cha kuchakata Mkonge na mara nyingi aina hii ya kiwanda hutumia mashine ndogo za **Raspado** kuchakatia mkonge. Mmiliki hununua Mkonge (majani) kutoka kwa wakulima wadogo na kuchakata kiwandani kwake kwa lengo la kutengeneza nyuzi (*sisal fiber*).

Mmiliki wa kiwanda atagharamika malipo yote kuanzia malipo ya Mkonge kwa mkulima, malipo ya wakataji Mkonge, usafirishaji wa Mkonge kwenda kiwandani,malipo ya wafanyakazi wa mashine,

malipo ya maji ya kuonyeshea fiber baada ya kuchakatwa, mafuta ya mashine, pamoja na chakula cha wafanyakazi. Baada ya Mkonge kuchakatwa na kuoshwa huanikwa na baadaye kuanuliwa na kufungwa katika mizigo midogo ya wastani wa kilo 20 kisha kuhifadhiwa tayari kwa kuuza kwa wanunuzi.

Kwa wastani mtu mwenye kiwanda kidogo cha mashine mbili huweza kuzashaliza wastani wa tani 2 (2,000kg) za sisal fiber kwa kila wiki ya uzalishaji, kwa matumizi ya mashine hizi kwa kawaida huzalisha grade ya SSUG ambapo kwa wastani wa bei ni Tsh 1,700,000 - Tsh 2,200,000 kwa tani moja (hii ni bei ya shambani kwa fiber ambayo haijaongezwa thamani yeyote). Bei hutokana na hali ya ubora wa fiber iliyozalishwa na pia hali ya soko huchangia zaidi bei kupanda na kushuka.

Kiujumla kwa wastani gharama ya uzalishaji wa tani moja huwa ni 75% - 85% ya mauzo. Mfano wa mauzo ya Tsh 2,000,000 kwa tani gharama inaweza kua Tsh1,600,000 (80%) na mmiliki kufanikiwa kupata faida ya Tsh400,000 (20%) na kwa mmiliki wa kiwanda aliye na mashine mbili huweza kuzalisha tani 2 kwa wiki, kwa bei ya Tsh2,000,000 kwa tani jumla ya Tsh 4,000,000 kwa tani zote mbili itamgharimu Tsh3,200,000 (80%) na anaweza kupata faida ya Tsh 800,000 kwa wiki baada ya mauzo ya mzigo wake. Kwa wiki mbili anaweza kupata faida ya Tsh1,600,000 na kwa mwezi anaweza kutengeneza zaida ya Tsh 3,000,000.

Mmiliki atafanikiwa kupata faida kama tu usimamizi utakua mzuri na wakutukuka kutoka shambani mpaka kiwandani kinyume na hapo kukitokea uzembe wowote basi mmiliki anaweza kupata faidi ndogo sana au hasara katika biashara yake.

Faida au hasara inaweza pia kushuka au kupanda kutokana na gharama za uendeshaji kushuka na kupanda. Mfano bei ya ununuzi wa Mkonge kutoka kwa mkulima, bei ya mafuta, bei ya chakula na hata bei ya soko kiujumla. Kwahiyo ni vyema mfanyabiashara kujaribu sana kupunguza gharama za uendeshaji ili kupata faida kwenye

biashara yake .

Mmiliki wa kiwanda anaweza pia akawa na mashamba yake mwenyewe ya Mkonge na hii hurahisisha zoezi zima la uchakataji wake binafsi na pia humuwezesha kununua majani kwa wakulima wenzake ili kuendelea na uzalishaji.

- ✔ **Binafsi mimi nipo kwenye kundi hili la wamiliki wa viwanda vidogo.**



TBF



TIBE



TBF



TIBE



III. Mnunuzi na Muuzaji wa kati wa Sisal Fiber

Hawa ni wafanyabishara wenye mitaji mikubwa kidogo ambao wanafanya kazi ya ununuzi wa sisal fiber kutoka kwa wazalishaji wadogo na baada ya kununua nyuzi hizi huziongeza thamani kwa kupiga kayamba. Kayamba ni zoezi la kubrush nyuzi kwenye mashine na kuchambua ili kupata nyuzi bora na nzuri. Baada ya zoezi hili nyuzi hunyooka vizuri na kuwa katika ubora nzuri, baada ya hapo nyuzi hupelekwa kwenye mashine ya kubania (*pressing machine*) kwa

lengo la kuziweka nyuzi katika ujazo wa mizigo mikubwa ya kilo kati ya 100 ,200 mpaka 250 ili iwe rahisi kwa usafirishaji wa mzigo mkubwa mara moja. Hii ndio hatua ya mwisho kwa wazalishaji maana baada ya hapa dealer huyo anaweza kupeleka mzigo wake kwa wanunuzi wakubwa, mfano Mohamed Dewji au anaweza kuuza kwenye viwanda vikubwa vinavyo tengeneza kamba, magunia n.k maana wao huhitaji fiber kwaajili ya shughuli zao za uzalishaji wa bidhaa zao.

Kwa dealer huyu ununuzi unaweza ukamgharimu Tsh2,000,000 mpaka Tsh 2,100,000 kwa tani kutoka kwa wazalishaji wadogo, gharama ya kupiga kayamba na kupress mzigo huweza kuchukua Tsh400,000 mpaka Tsh500,000 kwa tani moja na hii ikiwa imejumuisha gharama za usafiri, ushuru, wapakiaji na gharama ndogo ndogo kwa ujumla. Mzigo wa tani moja huweza kumgharimu dealer Tsh2,500,000 mpaka Tsh 2,600,000 baada ya kuongeza thamani fiber, kwa bei ambayo dealer hawa hupata sokoni baada ya kuongeza thamani ni kati ya Tsh2,800,000 mpaka Tsh3,200,000 kwa tani moja. Kwahiyo anaweza kupata faida ya Tsh300,000 mpaka Tsh 500,000 kwa tani moja na hapa grade inayohusika kwa sana ni SSUG. Kwa kawaida wafanyabiashara wa aina hii huwa na uwezo wa kuchukua tani 10 na zaidi hivyo huweza kupata faida ya Tsh3,000,000 mpakaTsh5,000,000 kwa mzunguko mmoja tu, faida nzuri hupatikana kwenye kundi hili maana ukubwa wa mtaji wako ndio ukubwa pia wa faida utakayoipata.

Biashara ya zao la Mkonge ni kama biashara nyingine kwahiyo umakini unahitajika sana maana unaweza kupoteza pesa nyingi kama umakini utakosekana. Sababu ambazo huweza kusababisha hasara kwenye mzunguko wa kazi ni kama wizi wa hali yeyote, ununuzi wa fiber zisizo na ubora unaotakiwa, kuchakachuliwa kwa mizani wakati wa zoezi la upimaji likiendelea na kushuka kwa bei sokoni nk.



TIBF



PDF



TBF



TIBF



TBF



TIBF

IV. Wanunuzi na Wauzaji wakubwa wa sisal fiber Nje ya Nchi (Soko la Dunia)

Hili ni kundi linalolenga matajiri /wafanyabishara wakubwa ambao wana uwezo mkubwa wa kiuchumi wa kununua fiber kutoka kwa dealers wa kati na kukusanya mizigo ya kutosha ya fiber kwa lengo la kuuza nje ya nchi kwenye soko la dunia. Kundi hili pia baadhi humiliki viwanda vikubwa vya uzalishaji wa fiber(*estate*) na mara nyingine pia humiliki viwanda vyao wenyewe vya kutengenezea bidhaa kama kamba, magunia,gypsum board nk.

Kundi hili hupata faida nzuri sana maana huuza bidhaa zao kwa fedha za kigeni nje ya nchi na huwa na uwezo wa kusafirisha mzigo mkubwa sana nje zaidi ya kontena 30 kwa mara moja lenye takribani ft 40 na

lenye uwezo wa kuingiza tani 27 mpaka 28. Pia kundi hili hukusanya fiber ya aina yeyote kulingana na uhitaji wa soko kwa wakati huo mfano UG,SSUG au TOW. Mfano mzuri unaonekana kwa mfanyabiashara Mohamed Dewji akiwa kama kinara wa biashara hii ya Mkonge kwa Afrika Mashariki.



V. Kiwanda kikubwa cha uzalishaji wa sisal fiber (*Estate*)

Viwanda vya namna hii vinaweza kumilikiwa na watu binafsi, Taasisi,

Mashirika na Serikali. Kundi hili linahitaji uwezo mkubwa sana wa kiuchumi wa kununua maeneo, kuyalima, kupanda pamoja na kununua mashine kubwa zinazohitajika kuendeshea kiwanda. Viwanda hivi huzalisha grade bora ya fiber(3L , UG na SSUG kwa uchache sanaa) kwasababu hutumia mashine kubwa kwenye uchakataji wake .

Viwanda hivi huwa na mashamba makubwa sana ya Mkonge takribani heka 5,000 na zaidi, mashine kubwa ya kuchakata mkonge (*corona machine*), magari na matreka ya kubebea Mkonge, mashine za kayamba, pressing mashine, visima vya maji vya kutosheleza shughuli zote za kiwandani pamoja na miundombinu yote inayohitajika kuendeshea kazi za kiwandani.

Viwanda hivi hununua pia majani kwa wakulima wadogo walio karibu na kiwanda kwa maelewano maalum mfano ushirika ama kumlipa mkulima fedha kamili baada ya kukata Mkonge wake .

Machine ya kuchakata mkonge huwa ni mashine kubwa yenye uwezo wa kulisha /kuchakata zaidi ya mita 120 kwa siku na ni mashine zenye mifumo ya maji ya kuoshea nyuzi za Mkonge vizuri kupelekea uzalishaji wa nyuzi bora zaidi.

Viwanda vya namna hii humiliki magari na matreka ya kubebea Mkonge kutoka shambani mpaka kiwandani kwa wastani wa trekta 3 mpaka 4, piki piki kwa wasimamizi na Viongozi wa kiwandani na shambani kwaajili ya usimamizi wa kazi zote kiwandani. Viwanda vya namna hii pia huwa na mashine zakutosha za kayamba na mashine kubwa ya kupress fiber kwa ajili ya kubania mizigo tayari kwa kuuzwa.

Kwa kawaida viwanda vya namna hii huwa na uwezo wa kuzalisha wastani wa tani 3 mpaka 4 kwa siku na hii nizaidi ya tani 90 mpaka tani 120 kwa mwezi, grade inayozalishwa hapa kwa wingi ni UG, na bei ya UG huwa ni kati ya Tsh 3,800,000 na Tsh 4,200,000 kwa tani moja. Mfano wa tani 90 kwa kila mwezi viwanda hivi huweza kufanya mauzo ya zaidi ya sh 360,000,000 (90*4,000,000) kila mwezi, hii ni

wastani wa zaidi ya bilioni 3 kwa mwaka.

Gharama zote za kiwandani huwa kati ya 20% mpaka 30% kwa mwezi hivyo hupelekea upatikanaji mzuri wa faida hata baada ya makato ya kodi na makato mengine ya kiserikali, gharama za kiwandani ni kama malipo ya wafanyakazi, mafuta ya magari, matrekta na pikipiki, umeme, chakula, matengenezo ya vifaa, manunuzi ya vipuli mbalimbali,usafishaji wa mashamba ya Mkonge wa kampuni na gharama ndogo ndogo za kampuni.

Kwa upande wa soko la fiber za aina zote ni kubwa sana, hivyo huwezi kupata shida kwenye uuzaji na mara nyingi watu huweka order kwenye viwanda hivi mapema kabla ya mzigo kuzalishwa. Viwanda hivi huuza fiber kwenye soko la ndani kwa uchache sana ila mara nyingi huuza mizigo yao nje ya nchi moja kwa moja kwa bei nzuri sana ya wastani wa sh 4.5m - 5m kwa kila tani kwa hiyo faida huwa maradufu kwa wamiliki.

Viwanda vikubwa vya namna hii huingiza mabilioni ya pesa kwa mwaka ,hapa serikali pia hupata mapato ya kutosha kutoka kwenye hivi viwanda na pia viwanda hivi hutoa ajira za kutosha kwa watu mbalimbali kwenye ngazi tofauti.

Changamoto kuu za viwanda hivi ni za kawaida, mfano mashine kuharibika, kukatika kwa umeme, wizi unaofanywa na wafanyakazi ambao sio waaminifu, uzembe kazini, kutapeliwa pesa na wanunuzi(uwaminifu), ubovu wa management pia husababisha sana katika upataikanaji wa hasara kwa kampuni hivyo basi ni lazima wamiliki wawe na timu bora ambayo itafanya kazi kwa kujituma na kwa ubora ili kutimiza malengo ya kampuni.

Mfano wa viwanda vikubwa vya Mkonge (*Sisal Esta*te) kwa Tanzania ni Kigombe Estate, Mwera Estate, Mwelya Estate, Hale Estate, Magoma estate ,Mgombezi estate ,Mnazi estate ,Mazinde estate, Maramba Estate, Makaya Estate, Mkumbara Estate, Kimamba Estate, Muheza Estate nk. Viwanda hivi vinapatikana kwa wingi kwa mikoa ya Tanga

na Morogoro.

- **Hitimisho**.

Kiujumla lengo kuu la uandaaji wa taarifa hii ni kutoa elimu kidogo kuhusu kilimo na biashara ya Mkonge hapa Tanzania na hii ni kwasababu inaaminika kuwa maarifa ni silaha (***information is power***) kwahiyo taarifa hii itamuongezea maarifa mtu yoyote kwenye uwanja wa fursa ya upambanaji katika maisha yake ya kila siku.

Katika biashara ya mkonge mtu yoyote anayo nafasi ya kujifunza na kuamua kuifanya katika ngazi yeyote hapa Tanzania.

Kwa mtu yoyote atakayevutiwa na kilimo na biashara ya Mkonge kiujumla anaweza akajifunza zaidi kwa kufika kwenye mashamba ya Mkonge yaliopo karibu na makazi yake na pia kwenye viwanda vya uzalishaji ili aweze kujionea kwa macho na kwa vitendo kuanzia Mkonge unavyolimwa na mpaka pesa inavyopatikana .

Takwimu (*Figures)* mbalimbali ambazo nimezielezea hapo juu ni takwimu (*Figures)*sahihi ambazo ninakutana nazo kila siku kwenye shughuli zangu na ndio bei zilizopo sokoni na wala sio takwimu (*figures)* za kufikirika. Ifahamike takwimu hizi zinaweza kuwa na utofauti kidogo kwa baadhi ya sehemu/maeneo kutokana na upatikanaji wa zao la Mkonge hapa Tanzania.

Biashara hii kwa Tanzania inafanywa kwa ukubwa na watu wenye asili ya India, waarabu,wazungu, wachina na watanzania kwa uchache na kwa ngazi za chini. Ni nyema tuhabarishane kuhusu fursa hii maana ina mzunguko nzuri wa pesa itayopelekea uchumi mzuri kwa wafanyabiashara na nchi kwa ujumla. Ndio maana hata Viongozi wetu kwa kumtolea mfano Mhe.Kassim Majaliwa (Waziri mkuu wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania) amehamasisha kilimo hiki kwa sababu ya uhitaji wa Sisal fiber duniani kuwa ni mkubwa sana.

Zao la mkonge ni miongozi mwa mazao ya mkakati yanayo ingizia pesa nyingi kwa wananchi na Serikali kwa ujumla. Lakini pia ikumbukwe kuwa yapo mazao mengine mfano Korosho, Parachichi, Chai na Kahawa ambayo Serikari inaendelea kuweka mkazo katika kilimo cha mazao hayo kwa sababu uhitaji wake ni mkubwa katika soko la dunia hivyo basi wananchi wanapaswa kuifanyia kazi fursa hii ili waweze kukua kiuchumi.

Najua katika nchi yetu kuna watu wenye uwezo mkubwa wa kifedha na wanatamani kufanya uwekezaji katika sekta mbalimbali hivyo basi ningewashauri wajaribu kuangalia fursa katika kilimo na biashara ya Mkonge.

Kwa wadau watakao pendezwa na zao la mkonge na biashara yake kiujumla wanaweza pia kupita kwenye kurasa hii ya instagram **(SISAL_FIBER_TZ)** kwa lengo la kujiongezea zaidi maarifa kuhusu biashara ya mkonge hapa Tanzania.

TIBE

Karibu shambani

From TIBE

Mawasiliano ; 0738-229894 (whatsapp)

; 0755-070038